

**JIMBO KATOLIKI LA MOROGORO  
SHULE YA SEKONDARI ALFAGEMS (S. 3874)  
S.L.P. 6083 – Morogoro**

Simu: 0689-783630 (Ofisi Taaluma) / 0789-978886 (Airtel Money)  
0689-783672 (Bweni la kike) / 0689-782670 (Bweni la kiume)  
[www.alfashule.ac.tz](http://www.alfashule.ac.tz)

**TARATIBU ZA KUJIUNGA NA KIDATO CHA KWANZA**

Ndugu ..... tunafurahi kukujulisha umepata nafasi ya kujiunga na kidato cha kwanza kwenye shule yetu iliyoko katika manispa ya Morogoro, kata ya Tungi, mtaa wa Mji Mwema (kati ya Msamvu na Nanenane). Karibu sana!

Hakuna malipo zaidi ya **ada ambayo ni:**

- (a) Kwa mwanafunzi wa kutwa Tsh. 600,000 kwa mwaka.
- (b) Kwa mwanafunzi wa bweni Tsh. 1,200,000 kwa mwaka.

Unaruhusiwa kulipa kwa mikupuo minne, yaani Tsh. 150,000, au 300,000 kabla ya kila nusu mhula, lakini bila robo hiyo hutapokewa.

Kwa usalama wa wote unaombwa **ulipie benki** (akaunti yenyne jina la shule iko MKOMBOZI C.B. ikiwa na namba 00120603517801; iko pia CRDB, namba 01J2077746000), si kwa mawakala wao wala kwa simu, **halafu vocha uilete shulenii** katika ofisi ya mhasibu upate risiti. Nje ya hapo usitoe pesa kwa yeyote, hata kama ni mwalimu wetu: malipo ya namna hiyo si halali, hivyo shule haihusiki nayo. Jihadhari sana!

Shule imekubaliwa kuwa wakala wa kampuni ya Airtel Money ili kupokea pesa kwa urahisi zaidi. Namba ni 0789-978886 na inatumika pia kwa mawasiliano.

Vilevile shule imekubaliwa kuwa wakala wa benki ya Mkombozi, isipokuwa utaratibu haujakamilika.

Unapewa siku 28 kulipa ada na kutuletea vocha ya benki; ukichelewa, nafasi yako atapewa mwininge, na wewe utahesabiwa mtu wa akiba hivi kwamba utaweza kupewa nafasi tena tarehe 16-1-2024 alfajiri kama zitakuwepo bado.

Masomo yataanza tarehe **9-1-2024**. Basi:

- (a) Ukitaka kuwa mwanafunzi wa kutwa ufile shulenii tarehe hiyo saa 1:15 asubuhi.
- (b) Ukitaka kukaa bweni ufile kabla ya saa 10:00 jioni ya tarehe iliyotangulia mwanzo wa masomo (kwa kuwa nafasi hazitoshi kwa wote, watapewa waliowahi kuleta ofisini mwetu vocha ya benki; nafasi zinaweza kwisha hata kabla ya tarehe hiyo).

Ulete Biblia (isipokuwa kama si Mkristo), kamusi ya Kiingereza, kivuli cha cheti cha kumaliza darasa la saba na vitu vilivyoordheshwa hapa chini:

**1. Sare** kama ifuatavyo (huruhusiwi kuleta nguo za aina nyininge):

- (a) Kwa wasichana:

- (i) Shati jeupe lenye maandishi ya shule
- (ii) Sketi ya rangi ya damu ya mzee (ifikie sentimeta 25 kutoka ardhini)
- (iii) Viatu vyeusi vyakama visivyo na visigino virefu
- (iv) Soksi nyeupe zisizo na urembo wowote
- (v) Sweta ya rangi ya damu ya mzee
- (vi) Kwa michezo: fulana yenyne maandishi ya shule, trakisuti na raba
- (vii) Masista wanaruhusiwa kuva sare ya shirika
- (viii) Waislamu, kwa ombi la mzazi/mlezi, wanaweza wakaruhusiwa kuva hijabu halisi nyeupe isiyo na pambo mradi wanyoe nywele zote.

- (b) Kwa wavulana:

- (i) Shati jeupe lenye maandishi ya shule
- (ii) Suruali ya rangi ya damu ya mzee
- (iii) Viatu vyeusi vyakama visivyo na visigino virefu
- (iv) Soksi nyeupe zisizo na urembo wowote
- (v) Sweta ya rangi ya damu ya mzee
- (vi) Kwa michezo: fulana yenyne maandishi ya shule, bukta ya buluu na raba
- (vii) Mabradha wanaruhusiwa kuva sare ya shirika.

**2. Kwa kukaa **bweni**:**

- (a) Fulana ya kijani yenyne maandishi ya shule
- (b) Nguo ya kulalia na ya kwenda bafuni
- (c) Mashuka na blanketi
- (d) Chandarua kilichotiwa dawa
- (e) Godoro la futi mbili unusu
- (f) Ndoo
- (g) Sanduku imara na salama
- (h) Taulo na vifaa vingine vyakama usafi
- (i) Sahani, bakuli, kikombe na kijiko
- (j) Nauli ya kurudi nyumbani wakati wowote.

**N.B. Ni lazima** mashati, fulana za shule, sketi, suruali na sweta vinunuliwe shulenii.

Biblia (Tsh. 22,000), kamusi (Tsh. 22,000), magodoro (Tsh. 42,000), mablanketi (Tsh. 15,000), mashuka (Tsh. 7,000), vyandarua (Tsh. 6,000), trakisuti (Tsh. 18,000), taulo (Tsh. 6,000), ndoo (Tsh. 3,500), begi (Tsh. 20,000), viatu (Tsh. 27,000), madaftari na kalamu vinapatikana shulenii kwa bei nafuu kama ilivyoonyeshwa katika mabano.